



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA MJI NJOMBE**



NTC/E:P/152/522/1B/121

31/10/2022

### **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA AJIRA YA MUDA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe anapenda kuwatangazia wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa, kuomba nafasi za kazi za muda kama zifuatazo:-

#### **MKUSANYA MAPATO-NAFASI 95.**

##### **Sifa za muombaJI;**

Awe na Elimu ya kidato cha Nne (Form IV) au kidato cha sita (VI), aliye hitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika fani yoyote kutoka chuo kinacho tambulika na serikali,

##### **KAZI / MAJUKUMU.**

- 1.Kukusanya Ushuru unaotokana na Mapato na tozo mbalimbali za Halmashauri
- 2.Kufanya Ukaguzi na uhakiki wa Malipo ya Ushuru Na tozo za Mazao na Maliasili katika Maeneo ya kazi.
- 3.kutunza mali na nyaraka zinazo husiana na Ukusanyaji wa Mapato
- 4.Kuchukua Hatua stahiki kwa yeyote atakae kiuka sheria na taratibu za Tozo na ukusanyaji mapato
- 5.Kazi zingine atakazo pangwiwa na muajiri.

#### **MENEJA MSAIDIZI WA STENDI-NAFASI MOJA (1)**

##### **Sifa za Muombaji.**

1. Awe muhitimu wa kidato cha Nne (IV) au Kidato cha Sita (VI) ,Awe na Stashahada(Diploma) ya Masoko,Uhasibu,uchumi na taaluma zinazofanana na hizo kutoka katika chuo kinachotambulika na serikali.
- 2.Awe na uwezo wa kupanga na kusimamia shughuli za kila siku,
- 3.Awe Mbunifu Katika kukusanya Tozo zilizopo stendi.
- 4.Awe na Uwelewa wa matumizi ya Kompyuta

##### **KAZI/MAJUKUMU**

- 1.Kusimamia usafi na ulinzi wa Stendi,
- 2.Kuhakikisha wapangaji wa stendi wanalipa kodi ya Pango kwa Wakati,
- 3.Kuhakikisha Mikataba Inatolewa kwa Wakati,
- 4.Kusimamia na kutoa taarifa kuhusu Hali ya Miundombinu na Vifaa vilivyopo stendi,
- 5.Kuzuia Na kutatua Migogoro katika maeneo ya Kazi.



## **MENEJA MSAIDIZI WA SOKO-NAFASI MOJA (1)**

### **Sifa za Muombaji.**

1. Awe muhitimu wa kidato cha Nne (IV) au Kidato cha Sita (VI) ,Awe na Stashahada(Diploma) ya Masoko,Uhasibu ,uchumi na taalma zinazofanana na hizo kutoka katika chuo kinachotambulika na serikali.
- 2.Awe na uwezo wa kupanga na kusimamia shughuli za kila siku,
- 3.Awe Mbunifu Katika kukusanya Tozo zilizopo Sokoni.
- 4.Awe na Uwelewa wa matumizi ya Kompyuta

### **KAZI/MAJUKUMU**

- 1.Kusimamia usafi na ulinzi wa Soko,
- 2.Kuhakikisha wapangaji wa soko wanalipa kodi ya Pango kwa Wakati,
- 3.Kuhakikisha Mikataba Inatolewa kwa Wakati,
- 4.Kusimamia na kutoa taarifa kuhusu Hali ya Miundombinu na Vifaa vilivyopo sokoni,
- 5.Kutoa Taarifa ya Bei za bidhaa sokoni Kila mwezi.
- 6.Kuzuia Na kutatutua Migogoro katika maemeo ya Kazi.


### **MSHAHARA.**

Kiwango cha mshahara kitategemea masharti ya Mkatoba.

### **MASHARTI YA MWOMBAJI**

1. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
2. Waombaji wote waambatanishe vyeti vya kuzaliwa.
3. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) Yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
4. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Taaluma, cheti cha kidato cha nne na cheti cha kuhitimu mafunzo,
5. Waombaji waambatishe Picha moja ya Passport size mbili ya hivi karibuni.

Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **13/11/2022** Siku ya Jumatatu saa 9:30 Alasili.

  
Kny: **MKURUGENZI**  
**GAMA E.Z.** HALMASHAURI YA MJI  
**KAIMU:MKURUGENZI** NJOMBE  
**HALMASHAURI YA MJI**  
**NJOMBE**

Nakala; Katibu Tawala (M)  
S.L.P 668,  
NJOMBE.

*Mbao za matangazo.*

Ofisi ya Mkurugenzi (TD), S.L.P 577 NJOMBE, Tovuti: [www.njombetc.go.tz](http://www.njombetc.go.tz), Simu: 026-2968833

Barua pepe: [td@njombetc.go.tz](mailto:td@njombetc.go.tz), Posti Kodi : 31 Barabara ya Ikisa, 59108 Mjimwema -Njombe